



# WEKA TAYARI

Weka tayari vitu vya dharura

## ORODHA YA VITUVYA DHARURA

- Redio inayotumia betri pamoja na betri vipuri
- Tochi pamoja na betri vipuri
- Mishumaa, kiberiti pamoja na viberiti visizorowa maji
- Tia maji katika vyombo vilivyo muhuri (10L kwa kila mtu)
- Vyakula visivyo vya kuharibika – vinavyotosha kwa siku 3-4
- Jiko la gesi pamoja na mafuta yanayoweza kusogezwa
- Kopo bati linalotumiwa kufungulia pamoja na vyombo
- Mchanganyiko wa visu vya mfukoni
- Vitu vya huduma ya kwanza pamoja na mwongozo wa
- Dawa
- Vifaa vya choo pamoja na usafi
- Nguo za kubadilisha pamoja na viatu vyenye kudumu
- Vitu maalum kwa watoto, wazee pamoja na watu wenye ulemavu
- Vyakula vya wanyama unaowalinda nyumbani, maji pamoja na mahitaji mengineo ya wanyama.
- Fedha taslimu (ATMs vyaweza kutopatikana)
- Nakala za kibinafsi (vyeti vya bima, picha n.k)
- Begi za plastiki vyenye kudumu (kwa nguo pamoja na vitu vyenye thamana n.k)
- Nambari za simu ya dharura



# SIKILIZA

Kaa kwa utaarifa

## LENGEZA REDIOYAKO KWENYE KITUO CHA REDIO KATIKA ENEO LAKO KWA TAARIFA MPYA

**ABC CAIRNS** 801 AM, 106.7 & 95.5 FM

**ABC CAIRNS** (MOSSMAN & PORT DOUGLAS) 639 AM, 90.1 FM

**ZINC CAIRNS** 102.7 FM

**4CA AM** 846 AM

**HOT FM** 103.5 FM

**SEA FM** 99.5 FM

**4AM PORT DOUGLAS** 1422 AM

**PORT DOUGLAS FM** 90.9 FM

[www.cairns.qld.gov.au/disaster](http://www.cairns.qld.gov.au/disaster)

## MAWASILIANO YA DHARURA YA BARAZA

Kwa maelezo **KABLA YA** kimbunga 4044 3044

Kwa maelezo **WAKATI WA** kimbunga 4044 3377

Kama ukihitaji mkalimani akusaidie kupata maelezo kuhusu maafa, kama vile kimbunga, tafadhali pigia simu Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (TIS Kitaifa kwenye 131450) na uwaulize wawapigie simu Baraza la Eneo la Cairns kwenye 40443044.

## Fuata Kituo cha Uratibu wa Maarifa kwenye



Facebook &



Twitter

## kwa dharura pigia simu 000 moja kwa moja.

Twatapangia mkalimani kwa ajili yako.

## Mawasiliano ya dharura

Polisi / Gari la wagonjwa / Moto **000**

Huduma ya Dharura ya Mkoa (State Emergency Services) (SES) **132 500**

Ergon Energy **132 296**

Main Roads (Barabara Kuu) **131 940**

# Kujitayarisha kwa vimbunga

Maelezo kwa wakazi na wageni



## MPANGO

Fanya mpango wa Dharura



## WEKA TAYARI

Weka tayari vitu vya dharura



## SIKILIZA

Kaa kwa utaarifa

Hatua ndogo za weza kufanya tofauti kuu duniani. Karatasi Rikaratasi Jimazosagwa.



MPANGO



WEKA TAYARI



SIKILIZA



## KIMBUNGA NI NINI?

Kimbunga ni dhoruba kali ya hari inayokuwa na upepo wenye nguvu pamoja na mvua nyingi na yaweza kusababisha uharibifu kina wa mali. Kituo cha 'jicho' au katikati ya kibunga ni eneo inayokuwa na upepo mwepesi pamoja na mara nyingi huwa na uwazi wa hali ya anga. Hata hivyo chungu; hii si mwisho wa kibunga, kwani upepo wenye uharibifu kutoka upande mwingine waweza kutokea.

Kaa ndani!

## AINA ZA KIBUNGA

AINA	UPEPO WENYE NGUVU ZAIDI	SIFA ATHARI
1	Chini ya 125 kph	Uharibifu kina wa nyumba; uharibifu mkuu kwa mimea, miti pamoja na misafara; hila zaweza kuinuliwa katika diko.
2	125-170 kph	Uharibifu mdogo wa nyumba; uharibifu kwa ishara; miti pamoja na misafara, uharibifu mkuu kwa mimea mingine, hatari kwa kushindwa kwa nguvu za umeme, hila ndogo zaweza kuinuliwa katika diko.
3	170-225 kph	Uharibifu kwa paa pamoja na miundo ya mali nyingine; misafara mingine pamoja na mimea yaweza kuharibiwa; uwezekano wa kushindwa kwa nguvu za umeme.
4	225-280 kph	Upotevu mkubwa wa paa pamoja na uharibifu wa miundo; misafara mingi kuharibiwa na kupeperushwa, hatari dhuru ya uchafu kwenye anga; kuenea kwa kushindwa kwa nguvu za umeme.
5	Zaidi ya 280 kph	Hatari kuu kwa uharibifu ulioenea.



## UANGALIFU WA KIBUNGA

Idara ya Hali ya Anga hutoa nakala ya Uangalifu wa Kibunga masaa 48 kabla ya wakati uliotabiriwa kibunga kutokea. Maelezo haya hurekebisha kila masaa 6.

## Onyo la Kibunga

Onyo la Kibunga hutolewa punde tu upepo wenye nguvu unapotarajiwa kudhuru jamaa wanaoishi pwani au kisiwani ndani ya masaa 24. Itakujulisha sehemu Kibunga kipo, harakati yake, kipo na nguvu ngani pamoja na utabiri wa maeneo ambayo yapo hatarini. Utabiri wa mvua nzito, mafuriko pamoja na ongezeko la dhoruba palipo na umuhimu.

Wakazi na wageni wanafaa kujitahadhari ili kuzuia na kujikinga kwa maisha na mali yao.



# MPANGO

Fanya mpango wa Dharura

## KABLA YA KIBUNGA

- Sikiliza redio yako (hakikisha kuwa unazo betri vipuri)
- Angalia kuwa vitu vya Dharura vipo tayari na karibu
- Funganisha au panga kila kifaa cha nje pamoja na samani
- Funika madirisha/milango kwa bao, au kwa mkanda wa ngundi kwenye kioo kwa mkanda wa ngundi pamoja na kufunga milango yote
- Hakikisha kuwa gari lako limejaa mafuta pamoja na kulihifadhi chini ya paa kama ikiwezekana
- Hakikisha kuwa mashua pamoja na misafara ipo kwenye gereji, au kama siyo, fanya hima kulisalamisha kwa kamba yenye nguvu kwenye hatua ya nanga
- Ondoka kutoka kwa misafara pamoja na hema
- Kama unatemelea eneo, ongea naye mtoa wa makazi kuhusu nini wafaa kufanya na wapi unafaa kuenda
- Jaza vyombo vya kunywa pamoja na bunde la kuongea na chombo cha takataka kwa maji – maji haya yaweza kutumika kuosha choo kama ugavi wa maji ukidhuriwa
- Fungia maji kama kukishindika nguvu za umeme
- Weka nakala muhimu pamoja na vitu vya gharama kwenye mifuko ya plastiki au vyombo vinginevyo visivyorowa na maji na uviweke kwenye sehemu salama
- Toa umeme pamoja na vifaa visivyo muhimu vinavyotumia umeme

## WAKATI WA KIBUNGA

- Endelea kusikiliza redio yako inayotumia betri kwa onyo pamoja na mawaidha
- Kaa ndani pamoja na kujiweka wewe na jamii yako kwa utulivu
- Jihifadhi katika sehemu yenye kudumu katika njengo, mara nyingi hii huwa ni kwenye bafu, choo au barabar ya ukumbi
- Magodoro pamoja na blanketi zaweza kukulinda
- Chungu jicho lililotulivu/katikati ya kibunga– Kaa ndani!

## BAADA YA KIBUNGA

- Kaa ndani mpaka ufahamishwa kwenye redio kuwa kibunga kimeshapita
- Kaa kado kabisa ya laini ya hatari! Kuwa chonjo kuwa laini za umeme zilizoanguka 'zinaumeme'
- Kaa kado na maji ya mafuriko

## DHORUBA YENYE ONGEZEKO NI NINI?

Dhoruba inayoongezeka ni ongezeko la kimo cha maji ya bahari inayohusika na vibunga. Kuongezeka kwa Dhoruba husababishwa na upepo wa juu unaosukuma ufuu wa bahari pamoja na upungufu wa shinikizo la hewa ya kawaida kutokana na dhoruba. Kibunga kinapofikia pwani upepo mwingi hupiga bahari na kusukuma maji juu ya maeneo ya pwani yaliyo chini zaidi, husababisha mafuriko, uharibifu wa nyumba pamoja na kukata njia za kuondokea.

Ramani kina zinazoonyesha maeneo yaliyo na ongezeko la dhoruba kwa kikanda cha Eneo la Baraza la Cairns hupatikana kwa kwenda kwenye tuvuti la Baraza:

[www.cairns.qld.gov.au/disaster](http://www.cairns.qld.gov.au/disaster)



## UTARATIBU WA KUTOKA KWA DHARURA

- Isipokuwa ushauriwe kuondoka, kaa ndani kila mara na ujiweke wewe na jamii yako kwa utulivu
- Sikiliza redio yako kwa maelezo ya kuondoka
- Kama upo kwenye eneo lenye ongezeko la dhoruba unasisitizwa kufanya mpango wa awali kwa makazi mengineo kwa muda kwenye jamii au marafiki katika "sehemu za juu zaidi", ukihitari kuondoka kwa ghafla
- Kama ikibidi kuondoka kwa ghafla, wafanyi kazi wa dharura waweza kukugongea mlango kwenye mtaa wako ili kukuelekeza kwenye mahali salama
- Baraza inayo Vituo vya Kuondokea vilivyoteuliwa kwa watu wasio na chaguo lingine. Hawaruhusu wanyama waliolindwa nyumbani, pombe au silaha
- Toa umeme kutoka vifaa vyote vyenye kutumia umeme /gasi kabla ya kuondoka
- Chukua vifaa vya Dharura nawe pamoja na shuka za kiulalia kwenye kitanda pamoja na kitambaa cha taulo kama ikiwezekana

**Kwa maelezo zaidi kuhusu kujitayarisha kwa vibunga, tembelea tuvuti ya Baraza**

[www.cairns.qld.gov.au/disaster](http://www.cairns.qld.gov.au/disaster)

